MAJUKUMU YAKO NI YEPI KATIKA SHUGHULI YA UKAGUZI WA POLISI?

Unaweza kuwasilisha habari/ripoti kuhusu afisa wa polisi kwa Tume Ya Ajira Kwa Polisi kabla Afisa mhusika kukaguliwa. Wasilisha habari/ripoti kwa Tume kuhusu afisa yeyote wa polisi ambaye:

- Amehusika na ukiukaji wa haki za kibinadamu ikiwemo ubaguzi ama mauaji ya kiholela, kudhulumu, kuwatia nguvuni watu kinyume cha Sheria na kutekeleza dhulma za kijinsia.
- Amehusika na ufisadi, biashara za ufisadi, uhalifu wa kiuchumi na uporaji wa mali ya umma
- Amehusika na ukiukaji wa Kifungu cha sita kwenye Katiba kuhusu uongozi na uadilifu; kwenye utendakazi wake kwa wakenya.
- Amesimamia kituo cha polisi ambapo haki za binadamu zilikiukwa ama zinaendelea kukiukwa. Amezembea kazini, ikiwemo kushindwa kusuluhisha kisheria malalamishi kutoka kwa umma, hivyo kuchangia kuongezeka kwa uhalifu. Habari au ripoti zote za malalamishi kwa tume lazima ziwe na: Anwani ya mtu/kundi linalowasilisha (majina,anwani, nambari za simu n.k)
- Maelezo ya afisa wa polisi mhusika (jina/anwani, kituo, hadhi/cheo chake n.k)
- Maelezo kamili ya malalamishi.
- Sahihi ya mtu/kundi linalowasilisha malalamishi.

National Police Service Commission (NPSC)

Pamoja tubadili huduma ya polisi kwa ufanifu katika utoaji huduma

Wasilisha habari/ripoti kwa:
The National Police Service Commission
5th Floor Skypark Plaza;
P.O. Box 47363-00100 Westlands Nairobi
Email: complaints@npsc.go.ke
Tel:+254-020-2186028/ +254 (020) 218 5989/
+254(020)2186061
Website: www.npsc.go.ke

Pamoja tubadili huduma ya polisi kwa ufanifu katika utoaji huduma

UTARATIBU WA UKAGUZI WA POLISI: MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

RUWAZA
Kudumisha hadhi na weledi katika huduma ya polisi.

MAARUBU
Kuboresha usimamizi wa nguvu kazi kwa ufanisi wa huduma ya polisi

AMALI
Huru na uadilifu
Uwazi na uwajibikaji
Kuheshimu anuwai zetu na usawa

UKAGUZI NI NINI?

Utaratibu huu unahusisha ukaguzi wa wafanyikazi wa umma kwa misingi ya maadili na uzoefu wa kazi ili kubaini bayana ikiwa wanastahili kuendelea kuhudumu katika ofisi za umma.

MALENGO YA KUWAKAGUA POLISI NI YEPI?

- Kuimarisha imani ya wananchi kwa Huduma ya Polisi kwa Taifa;
- Kuhahakisha kuwa Huduma ya Polisi Kwa Taifa inaambatana na Kifungu cha sita cha katiba ya Kenya na ibara ya 232 ya Katiba inayoangazia kanuni za huduma kwa umma.

KWA NINI POLISI WAKAGULIWE?

Kuna Sheria tatu muhimu zinazoangazia zoezi zima la kuwapiga msasa maafisa wa Huduma ya Polisi.

- Sheria ya Huduma ya Polisi kwa Taifa (National Police Service Act),
- Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Polisi (National Police Service Commission Act),
- Mamlaka Huru ya Kusimamia Polisi (Independent Policing Oversight Authority Act).

Kulingana na Sheria ya Huduma ya Polisi kwa Taifa, kifungu cha 7(2) na (3), maafisa wote wa polisi watapigwa msasa kutathmini iwapo wanastahili, na watasalia tu kwenye Huduma ya Polisi kwa Taifa iwapo watafaulu. Sehemu hiyo pia inaelezea kuwa Tume ya Huduma kwa Polisi ndiyo taasisi ya pekee iliyo na jukumu la kufanya ukaguzi huu.

NANI ATAPIGWA MSASA?

“Maafisa wote wa polisi waliokuwa wakihudumu kabla ya kubuniwa kwa Sheria ya Huduma ya Polisi kwa Taifa 2011; maafisa na wafanyikazi wa Kikosi cha Polisi wa kawaida na wale wa Utawala, kilichoanzishwa chini ya sheria ya Polisi Kifungu cha 84 na Sheria ya Polisi wa Utawala Kifungu cha 85 mtawalia, wakiwemo maafisa wanaohudumu na idara ya jinai.”

NI KANUNI ZIPI ZINAZOSIMAMIA UPIGAJI MSASA WA MAAFISA WA POLISI?

- Ukaguzi utapiga msasa wajibu na uadilifu wa afisa wa polisi binafsi
- Utaratibu utakaotumika utakuwa sawa kwa maafisa wote wanaokaguliwa.
- Ukaguzi utatilia maanani maadili na kanuni kwenye Ibara za 10, 27, 47, 50 na 232 za Katiba ya Kenya;
- Ukaguzi utatilia maanani Ibara ya 238 ya Katiba ya Kenya iniyoangazia usalama wa taifa. Ukaguzi utatekelezwa kwa njia ya uwazi na kwa malengo yanayo eleweka na yanayoweza kuthibitishwa.

UKAGUZI UTAFANYWA HADHARANI AMA FARAGHANI?

Ukaguzi na mahojiano yatafanyika hadharani. Baadhi ya vikao vya Tume huenda vikaendeshwa faraghani kwenye hali maalum ili kulinda siri ya mtu yeyote ama iwapo ni kwa manufaa ya haki au maslahi ya usalama wa taifa.

NI MIZANI IPI ITATUMIWA KUMPIGA MSASA AFISA WA POLISI?

Mizani ya ukaguzi kuamua iwapo afisa wa polisi anastahili kusalia itazingatia rekodi ya utendakazi wake, utaalamu, na jinsi anavyofanya kazi sasa na awali na kwenye wadhfa wowote ule aliowahi kushikilia. Ili kuamua iwapo afisa anastahili kazi, tume itazingatia yafuatayo:

- Iwapo afisa anatimiza maadili na masharti ya kikatiba na Sheria za uteuzi na ajira ya Huduma kwa Umma
- Historia ya utenda kazi wa afisa anayekaguliwa
- Uadilifu na uwezo wa Afisa anayekaguliwa kuelezea kiini cha utajiri wake
- Rekodi au historia ya Afisa anayekaguliwa ya kulinda haki za kibinadamu.

AFISA ANAWEZA KUSTAAFU KWA HIARI?

- Afisa wa polisi anaweza akastaafu kwa hiari kutoka kwenye huduma kabla ya kupigwa msasa na atafahamisha Tume kuhusu uamuzi huo
- Afisa ambaye amestaafu kwa hiari hatapigwa msasa
- Kwa Afisa atakayestaafu kwa hiari, Tume itashughulikia maswala ya kustaafu kulingana na sheria.

MAMLAKA YA TUME YA AJIRA KWA POLISI KATIKA UKAGUZI NI YAPI?

Tume na kila jopo litakaloundwa chini ya kanuni za ukaguzi litakuwa na mamlaka yote ya kutekeleza majukumu yake.Hayo ni pamoja na:

- Kukusanya habari mwafaka,ikiwemo kupata ripoti, rekodi, nyaraka ama habari yoyote kutoka kwa vyanzo/ duru, ikiwemo idara za serikali na kushurutisha kutolewa kwa habari hizo wakati zinapohitajika;
- Kuhoji mtu yeyote, kundi ama wanachama wa kikundi au taasisi;
- Kuuliza maswali kwa kusudi la kutekeleza majukumu yake chini ya kanuni na taratibu za Tume;
- Kufanya uchunguzi kutambua ukweli wa habari zilizopokelewa.

TUME YAWEZA KUBUNI MAJOPO YA UKAGUZI?

- Tume inaweza kubuni majopo yatakayo jumuisha watalamu wa maswala mbalimbali.
- Iwapo jopo halina mwanachama wa Tume, jopo hilolitatuma mapendekezo yake kwa Tume kwa maamuzi ya mwisho.
- Tume inaweza kuanzisha majopo yatakayo jumuisha wanachama wake na wataalamu wengineo kwa kusudi la kuamua rufaa zote zitakazotokana na ukaguzi huu.
- Tume na/ama jopo yaweza kuandaa vikao wakati na mahali jinsi Tume/ Jopo itakavyoamua.

NINI KITAKACHOFANYIKA IWAPO AFISA ATASUSIA UKAGUZI?

Ikiwa Afisa atasusia kufika kwenye jopo ama tume ili kukaguliwa, ama akatae kutii agizo la Tume kwa mujibu wa utaratibu wa ukaguzi huu, ataondolewa kutoka kwa Huduma ya Polisi kwa Taifa.

MBONA UKAGUZI WA POLISI NI MUHIMU KWAKO KAMA MKENYA?

Ukaguzi wa polisi ni fursa nzuri kwa taifa kurejesha utaalamu na imani ya wananchi kwa Hudumu ya Polisi kwa Taifa. Inatarajiwa kuwa ukaguzi huu utabadilisha idara ya polisi kuimarisha usalama wa umma.

Pamoja tubadili huduma ya polisi kwa ufanifu katika utoaji huduma
Pamoja tubadili huduma ya polisi kwa ufanifu katika utoaji huduma